- Kanuni za Mahakama ya Rufaa Tanzania; Tangazo la Serikali Na.102 la mwaka 1979.
- Kanuni za Mwenendo wa Mashauri ya Serikali (na taratibu); Tangazo la Serikali Na.376 la mwaka 1968.
- Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria ya Usimamiaji Haki na Matumizi yake [Sura ya 1 kama sheria ilivyorekebishwa mwaka 2002];

**Mafanikio**

Kumekuwa na mafanikio mbalimbali tangu mradi ulipoanza mwaka 2006, baadhi ya mafanikio hayo ni:-

i. Kutengenezwa Waraka wa Majumuisho mwaka 2006;

ii. Kupatikana kwa maoni kupitia Waraka wa Majumuisho kutoka kwa wadau mbali mbali wakiwemo Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Majaji wa Mahakama Kuu, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea;

iii. Mapitio ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 1979, ambayo yamepelekea kuundwa kwa Kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 2009; na

iv. Kupatikana kwa mtaalam ambaye atayafanyia kazi Waraka wa Majumuisho wa Mfumo wa Haki za Madai na baadaye kutoa rasimu ya marekebisho ya sheria na kanuni zilizoainishwa katika Waraka huu ili kutatua matatizo yaliyobainishwa katika Mfumo wa Haki za Madai

*Imeandaliwa na:*

***TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA***

*Jengo la Haki*

*Mtaa wa Luthuli*

*S.L.P. 3580*

*Simu: +255 22 211387/2123533*

*Nukshi: +255 22 2123534*

*Barua pepe: lrct@irct.or.tz*

*© LRCT 2010*

***KWA UDHAMINI WA PROGRAM YA KUIMARISHA MAZINGIRA YA BIASHARA TANZANIA (BEST)***

Printed By Rainbow Printers, Email: info@rainbowprinters.co.tz

**PROGRAM YA KUIMARISHA MAZINGIRA YA BIASHARA TANZANIA**

**(BEST)**

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**



# MAPITIO YA MFUMO WA HAKI ZA MADAI

Mfumo wa Haki za Madai ni sehemu ya mfumo wa haki kutekeleza, kurudisha na kulinda haki binafsi. Kwa maneno mengine, mfumo wa haki za madai unahusu utatuzi wa migogoro baina ya watu binafsi au taasisi lakini haujihusishi na makosa ya jinai. Mfumo wa haki za madai unahusisha migogoro ya kibiashara, madai ya mtu binafsi na migogoro kati ya mtu binafsi na serikali.

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inafanya mapitio ya Mfumo wa Haki za Madai kwa kuwa ni wazi kwamba, mazingira ya kibiashara ya nchi yoyote hutegemea mfumo wa utatuzi wa migogoro ambao ni wenye ufanisi, madhubuti na wenye kuingilika. Mfumo wa Haki za Madai ambao ni madhubuti na wenye kuingilika unawezesha utatuzi wa migogoro kwa haraka na gharama nafuu. Utaratibu huu utawezesha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa haki kwa Watanzania wote.

Kwa kufanyia mapitio Mfumo wa Haki za Madai, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inatekeleza malengo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania katika kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wote kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoeleza juu ya utoaji wa haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi na kutochelewesha haki bila sababu ya msingi, Kutoa fidia ipasayo kwa watu walioathirika kutokana na makosa ya watu wengine, kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro na kutoa haki bila ya ugumu wa utekelezaji (undue technicalities).

**Jukumu la Tume ya Kurekebisha Sheria katika Mapitio ya Mfumo wa Haki za Madai.**

Katika mradi huu wa Mapitio ya Haki za Madai, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inalenga kufanya mapitio ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai Tanzania pamoja na sheria na kanuni nyingine zinazohusiana na taratibu za madai, kufanya mapitio ya muundo uliopo sasa wa usimamizi wa mashauri ya madai, kuchunguza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwenye mahakama; na mwisho kabisa kutoa mapendekezo juu ya marekebisho ya Mfumo wa Haki za Madai unaokusudia kuendeleza uharaka na ufanisi wa kutatua migogoro ya madai kwenye mahakama za Tanzania.

**Matatizo yaliyopo kwenye Mfumo wa Haki za Madai**

Mfumo wa Haki za Madai una changamoto mbalimbali zikiwa ni pamoja na:-

- Ugumu wa sheria na kanuni zinazohusu mfumo wa madai na wadaawa kutokuelewa namna ya kuendesha mashauri ya madai
- Utaratibu wa kuongeza muda wa kupeleka utetezi haupo wazi na hivyo kusababisha kuchelewesha kusikilizwa kwa kesi.
- Kanuni zinazohusiana na kuongeza muda wa kupeleka utetezi hazijaelezewa vizuri.
- Ucheleweshaji wa nyaraka za Mahakama ni tatizo ambalo husababisha msongamano wa mashauri Mahakamani kutokana na kucheleweshwa kwa usikilizaji wa mashauri.
- Gharama za uendeshaji wa mashauri ni kubwa kwa Watanzania walio wengi.
- Mfumo wa haki za madai haueleweki na kwa kawaida ni vigumu kujua shauri litagharimu kiasi gani na litachukuwa muda gani kumalizika.
- Taratibu za mahakama hazieleweki kwa Watanzania walio wengi na mfumo uliopo sasa ni wa upinzani sana.

**Sheria na Kanuni Zitakazorekebishwa chini ya Marekebisho ya Mfumo wa Haki za Madai.**

Mradi huu hautafanyia kazi mapitio ya sheria zote zinazihusu mfumo wa madai ila ni baadhi tu ya sheria na kanuni zilizoainishwa na Waraka wa Majumuisho (Position Paper) wa 2006 kwa ajili ya mapitio nazo ni;-

- Sheria ya Mahakimu [Sura ya 11 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Ukomo [Sura ya 10 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai [Sura ya 33 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Usuluhishi [Sura ya 15 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ua Ushahidi Tanzania [ Sura ya 6 ya marekebisho ya mwaka 2002]
- Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali [ Sura ya 5 ya marekebisho ya mwaka 2002]
- Sheria ya Mamlaka ya Rufaa [Sura ya 141 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Mabaraza ya Kata [Sura ya 7 ya marekebisho ya mwaka 2002].